BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Nane – Tarehe 08 Disemba, 2023.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora,

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, Nam.12 ya 2019 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar Kusimamia Huduma za Serikali Mtandao Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar, Nam. 3 ya 2011 na Kutunga Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kwa ajili ya Kutoa Msaada wa Kifedha kwa Wanafunzi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

75. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Kuna muelekeo na mpango gani mkakati kwa Wizara yako katika kuhamasisha wawekezaji kuweza kuwekeza kwenye viwanda vya kuchakata matunda.

81. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    (a) Kitakwimu ni taasisi au kampuni ngapi ambazo zinahusika na suala la kuwasafirisha wafanyakazi wa majumbani nchi za nje ambazo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inazitambua rasmi.

    (b) Je, ni wafanyakazi wangapi kwa sasa wamepata ajira hizo kisheria.

    (c) Je, ni utaratibu upi unaotumika kuwapa vibali na ruhusa.

### Wizara ya Afya:

18. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya huduma ya 'Customer Care' katika vituo vya afya na hospitali zetu.

    (a) Je, Wizara yako imeandaa mpango gani wa mafunzo ya 'Customer Care' kwa watendaji wake.

    (b) Je, ni kwanini watendaji hawa wamekosa mafunzo ya 'Customer Care' kwa muda mrefu.

    (c) Je, Wizara yako inatoa kauli gani juu ya changamoto ya kukosekana kwa huduma ya 'Customer Care' kwa watendaji wake walio wengi.

50. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

'Methadone' ni dawa mbadala kwa watumiaji wa madawa ya kulevya na pale wanapoikosa huwa wanaathirika kimwili, kiakili na kisaikolojia.

Je bado 'Methodone' inaendelea kuwa mbadala halisi au kuna uwezekano mwengine wa kupata dawa mbadala zenye ubora zaidi ya 'Methodone'.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

44. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Matatizo yanayotokana na elimu yamekuwa yakielezwa kwenye ripoti na tafiti mbali mbali.

Je, ni ripoti na tafiti zipi ambazo Wizara mmeweza kuzipokea na kuzifanyia kazi katika kupata masuluhisho bora ya mabadiliko ya elimu.

79. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

(a) Je, ni kozi zipi za masomo ya elimu ya juu ambazo Wizara yako imezipa kipaumbele kwa kuwapatia udhamini na mikopo nafuu wanafunzi watakaochukua masomo hayo.

(b) Je, ni vigezo gani vya msingi vinazingatiwa katika uteuzi wa vipaumbele vya kozi hizo.

(c) Je, ni kwa kiasi gani malengo hayo yanatimia.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

69. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Mnara Kibutu uliopo eneo la kihistoria la Mangapwani ni miongoni mwa alama muhimu za historia ya nchi yetu ukitumika kuongoza wafanyabiashara wa magendo ya watumwa baada biashara hiyo kufungwa rasmi katika soko kuu la utumwa Mkunazini.

Je, ni kwa kiasi gani mnara huu unatunzwa na kuhifadhiwa kwa maslahi ya kuwarithisha vizazi na vizazi.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

70. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Zanzibar ina maeneo mengi ya kihistoria yanayotokana na mabaki yaliyozama chini ya ardhi na hata baharini.

Je, Serikali inachukua jitihada gani katika kutafuta wahisani wa kuiwezesha Idara ya Mambo ya Kale kufanya zoezi hili ili kuendelea kuibua historia yetu na kuihifadhi.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora,**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar, Nam.12 ya 2019 na Kutunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar Kusimamia Huduma za Serikali Mtandao Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo - Kusomwa wa mara ya Kwanza

**Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar, Nam. 3 ya 2011 na Kutunga Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kwa ajili ya Kutoa Msaada wa Kifedha kwa Wanafunzi na mambo mengine yanayohusiana na hayo - Kusomwa wa mara ya Kwanza.

## V. HOJA YA MJUMBE:

**Mhe Asha Abdalla Mussa.**

Hoja Binafsi ya Mjumbe kuhusu Kuunga mkono Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 katika kipindi cha miaka mitatu ya awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Zanzibar,
08 Disemba, 2023.

(Raya Issa Msellem)
**KATIBU WA BARAZA**